

Ndege za Karatasi



Hatua na maelezo fatilizi:

1

Kunja karatasi nusu mbili sawa sawa kwa urefu

2

Kunja kona moja katika kila nusu mbili za hapo mwanzoni

3

Katika kila kona moja kutoka na hizo nusu mbili, ongeza kukunja zaidi ili nusu uliyokunjwa na ile haikuikunja zitoshane sawa sawa

4

Zilete sehemu zote zilizo kunjwa hadi katikati

5

Tengeneza mabawa ya ndege kwa kukunja kuelekeza chini

6

Ndege iko tayari kupeperushwa!!



Tucheze
Kujifunza

Je unaweza kukisia zoezi litakalofuata? ▶
Kuna njia moja tu ya kujua zaidi. Ni kufuatilia ilani mahsusi za TuKu!



Jinsi ya Kutengeneza Kibonzo Cha Kuvaliwa Mkononi



Hatua na maelezo fatilizi:

1

Chukua soksi na
uivae kwenye
mkono



2

Kwa kutumia vidole
vingine na kidole
gumba, tengeneza
uso na mdomo kwa kucha
kwa kupitisha mkono
sehemu ya soksi iliyo wazi



3

Kwa usaidizi
wa msimamizi
unaweza kushona sehemu
za macho na mkono ili
kupendeza zaidi



Tucheze
Kujifunza

Je unaweza kukisia zoezi litakalofuata? ►
Kuna njia moja tu ya kujua zaidi. Ni kufuatilia ilani mahsusi za TuKu!



Kutengeneza Gari la Watoto la Kuchezea



Hebu lilete gari unalolienzi katika maisha yako!

1

Tengeneza gari la kuchezea la watoto kwa kutumia chupa za plastiki, mbaao laini laini au mabokisi ya maziwa na pia visoda kama magurudumu

2

Buni garaji au sehemu ya kugesha magari haya ya kuchezea ya watoto kutokana na vitu visivyo kuwa na madhara kwa mazingira

3

Peleka magari haya ya kuchezea ya watoto ili kujua zaidi lipi laenda kwa kasi zaidi kushinda mengine au linalohimili kwenda masafa ya mbali bila kuleta matatizo




**Tucheze
Kujifunza**

Je unaweza kukisia zoezi litakalofuata? ►
Kuna njia moja tu ya kujua zaidi. Ni kufuatilia ilani mahsusi za TuKu!



Kuchora Kivuli



Hatua na maelezo fatilizi:

1

Tafuta kitu chochote
ukipendacho
ili kukichora

2

Weka kitu ulichokipenda
juu ya karatasi safi na
uelekeze sehemu ya
jua ili kuweza
kuona kivuli chake

3

Kwa kutumia kalamu ya wino
au penseli (kalamu ya risasi)
fuatilia kwa kuchora nje
ya kivuli kitokanacho
na kitu ukipendacho,
unaweza kutia nakshi kivuli
ulichokichora kwa rangi
kadha wa kadha



Tucheze
Kujifunza

Je unaweza kukisia zoezi litakalofuata? ►
Kuna njia moja tu ya kujua zaidi. Ni kufuatilia ilani mahsusi za TuKu!



Mchezo wa Kubingirisha Chupa za Maji



Hatua na maelezo fatilizi:

1

Kusanya chupa tano, saba au kumi, juu ya kila chupa andika nambari kubwa kubwa

2

Jaza kila chupa nusu maji au mchanga, zipange chupa ili kutengeneza umbo la pembe tatu

3

Kila mmoja wa watoto wachezao, apewe fursa ili kibingirisha mpira kulenga hizo chupa ili kuona ziangukavyo



Tucheze
Kujifunza

Je unaweza kukisia zoezi litakalofuata? ►
Kuna njia moja tu ya kujua zaidi. Ni kufuatilia ilani mahsusi za TuKu!



Kuruka Miraba



Maagizo:

1
Chora miraba sakafuni au mchangani

2
Kuanza mchezo, mfanye mtoto wako atupe jiwe ndogo kwenye mraba 1

3
Ruka mraba 1 na uguse mraba 2. Ruka kwenye miraba mingine mpaka uwe nyuma ya mraba 2. Inama uchukue jiwe and uruke kwa mraba 1

4
Mtu anayefuata anapaswa kutupa jiwe lao kwenye mraba 2 na kurudia mchakato

5
Endelea kucheza ukibadilishana na kutupa jiwe lako kwenye namba tofauti hadi mawe yatakapowekwa kwenye kila mraba



Tucheze
Kujifunza

Je unaweza kukisia zoezi litakalofuata? ►
Kuna njia moja tu ya kujua zaidi. Ni kufuatilia ilani mahsusi za TuKu!



Kutengeneza Fumbo



Maagizo:

1

Chora picha yenye rangi kwenye kipande kikubwa cha karatasi

2

Kata picha hiyo angalau katika vipande hamsini vya mafumbo

3

Weka vipande vya mafumbo vilivyokatwa ndani ya mfuko wao vyenyewe na uutingishe ili kuchanganyisha vipande hivyo

4

Badilishana mafumbo yako na rafiki yako

5

Sasa furahia kutengeneza picha ya awali



Tucheze
Kujifunza

Je unaweza kukisia zoezi litakalofuata? Kuna njia moja tu ya kujua zaidi. Ni kufuatilia ilani mahsusi za TUKU!



Anzisha Duka Lako Mwenyewe



Maagizo:

1

Waweza kuigiza wahusika tofauti tofauti, yaani, mnunuzi, mtunza fedha muuzaji wa dukani na mlinzi

2

Ainisha na kupanga bidhaa dukani kwa kuweka vitambulisho vya bei kwenye kita bidhaa

3

Kama mmiliki wa duka, unda mauzo au ofa kwa bidhaa na kuhimiza wanunuzi wazinunue

4

Tumia maneno kama vile karibu, baada yako, tafadhali, asante, kwaheri, na kadhalika unapoigiza



Tucheze
Kujifunza

Je unaweza kukisia zoezi litakalofuata? ►
Kuna njia moja tu ya kujua zaidi. Ni kufuatilia ilani mahsusi za TuKu!



Ramani ya Ujirani



Maagizo:

1

Zungumza na rafiki yako kuhusu maana ya ramani. Inatumiwa vipi? Inabeba habari gani? Ikiwa una ramani, ionyeshe na muijadili

2

Chora ramani ya ujirani wako. Husisha minara inayojulikana kwenye ramani yako, kama vile maduka, nyanja, nyumba ya jirani ama rafiki, shule, na kadhalika

3

Angalia usahihi wa ramani hiyo. Tembea katika ujirani kuangalia kwamba habari kwenye ramani hiyo ni sahihi na ufanye marekebisho inavyohitajika



Tucheze
Kujifunza

Je unaweza kukisia zoezi litakalofuata? ►
Kuna njia moja tu ya kujua zaidi. Ni kufuatilia ilani mahsusi za TuKu!



Mpira Unaozungumza



1

Anayeanza kwa mpira aigize neno linaloonyesha kitendo (kitenzi) mfano, kuweka mikono pamoja, kufungua mikono, kurudia kwa haraka

2

Mtu mwingine ajaribu kubahatisha kitendo kinachigizwa. Mtu huyu aendelee kubahatisha hadi pale atakapokuwa sahihi. Akishakuwa sahihi, aurushe mpira kwa mtu wa pili

3

Endelea na mchezo huu hadi kila mmoja apate nafasi au hadi kila mmoja apate nafasi tano. Je, ni vitenzi vingapi tofauti ambavyo waigizaji walibahatisha wakapata?



Tucheze
Kujifunza

Je unaweza kukisia zoezi litakalofuata? ►
Kuna njia moja tu ya kujua zaidi. Ni kufuatilia ilani mahsusi za TuKu!

